**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

MFARANYAKI SEKONDARI
S.L.P 899
**SONGEA**
Email:mssf06@gmail.com

+255753524544
MSIMBO: S3248
KUMB NA MFSS/S.3031/F1/2020

# FOMU YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

**JINA LA MWANAFUNZI: ......................................................................**

## 1) UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule hii ya Sekondari ya Mfaranyaki iliyoko Kata ya Mfaranyaki, Manispaa ya Songea km 1 magharibi ya stendi kuu ya Mji wa Songea.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021.

## 2) MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. SARE ZA SHULE

(I) Suruali mbili (02) kwa wavulana rangi ya Kijani mgomba na sketi mbili (2) rangi ya njano ya karoti kwa wasichana. **(Kwa wavulana suruali ni lazima ndefu na zisizobana na kwa wasichana sketi ziwe pana na ndefu zikaribie visigino na Rangi ya suruali na sketi izingatie kipande cha kitambaa ulichopewa).**

(II) Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi kwa wavulana na wasichana.

(III) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

(IV) Soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana na ziwe ndefu

(V) Sweta rangi ya kijani kibichi (shingo "V")

(VI) Rangi ya Hijabu kwa wasichana wa kiislamu ifanane na sare ya shule (nyeupe)

(VII) Sare ya michezo kwa shule hii ni T-shirt ya michezo rangi nyeupe/kijani kwa wavulana na wasichana na bukta ya bluu kwa wavulana na tracksuit ya bluu kwa wasichana. Aidha raba ya michezo kwawote.

### B. VIFAA VYA DARASANI

(i) Daftari kubwa walau 12 aina ya "Counter Books Quire 2, 3 au 4

(ii) Mkebe, kalamu za wino mweuzi au bluu, penseli na rula.

(iii) Kamusi/ dictionary

(iv) Begi la kubebea vifaa vya darasani.

### C. CHAKULA NA MATIBABU KWA WANAFUNZI

Wanafunzi wa kutwa wanagharamiwa na wazazi chakula chao na matibabu. Chakula ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma, kiafya na kinidhamu. Hapa shuleni wazazi huchangia chakula cha mchana kwa watoto wao kupitia kamati ya wazazi. Ufanunuzi wa suala hilo utatolewa na kamati ya wazazi kwenu hapo baadaye.

Scanned with CamScanner

**D. MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU**

Wazazi wanapaswa kuangalia na kuwapatia vijana wao mahitaji yote ya kibinadamu kwa mfano mahitaji ya kimaumbile kwa wasichana.

**3) SHERIA NA KANUNI MUHIMU**

**A. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.**

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa masomo au nje ya mipaka hiyo kwa kibali maalumu.
- Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali za Umma.

**B. Yafuatayo ni makosa ambayo baada ya kuthibitishwa yanaweza kusababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja:-**

- Wizi
- Uasherati na ushoga
- Ulevi, uvutaji wa bangi na utumiaji wa madawa mengine ya kulevya
- Kupiga au kupigana
- Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- Kuoa au kuolewa
- Kudharau Bendera ya Taifa au wimbo wa Taifa
- Kusababisha mimba.
- Kuwa na mimba au kutoa mimba
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
- Utoro wa muda mrefu
- Makosa ya jinai

**Kumbuka mwanao anapaswa kujaza fomu zote kwa ukamilifu na kuzirejesha kwa mkuu wa shule. Pia tarehe 13/1/2021kutakuwa na kikao cha wazazi tafadhali fika bila kukosa kwa maandalizi ya kitaaluma ya mwanao.**

**NB: IMEAGIZWA KUWA FOMU YA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM) ITAJAZWA KATIKA HOSPITALI YA MANISPAA YA MJIMWEMA TU NA SI VINGINEVYO**

**KARIBU SANA MFARANYAKI SEKONDARI**
**AHSANTE**

**RAYMOND F. CHENGULA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MFARANYAKI
S.L.P.899 . SONGEA

Scanned with CamScanner

**FOMU "B"**

**AHADI YA KUTEKELEZA SHERIA, KANUNI MUHIMU NA WAJIBU**

**A. MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………………… nakubali nafasi niliyopata katika shule ya Sekondari Mfaranyaki kuanza elimu ya Sekondari. Ninafahamu kuwa ninagharamiwa na Taifa kupata elimu msingi bila malipo na wazazi wangu wanawajibika kunipa na nitakuwa Mwanafunzi mwaminifu katika kutimiza na kufuata sheria za shule na kushirikiana na wenzangu katika shughuli zote za shule.

**……………………………** **Tarehe: ……………………………………**

**Sahihi ya Mwanafunzi**

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………. nimesoma yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampa mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika fomu hii na barua zote zitakazomhusu mtoto wangu.

Ripoti na barua zote zinazomhusu mtoto wangu zitaletwa kwangu kwa anwani hii

Jina la Mzazi/Mlezi …………………………………………………………

S.L.P ……………………………………………………………………………

Namba ya Simu ……………………………………………………………..

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……………………...... Tarehe …………………………

**UTHIBITISHO WA MWENYEKITI WA MTAA**

Mimi Mwenyekiti wa mtaa wa ………………………………………………….. nathibitisha kumfahamu Bwa/Bibi ……………………………………………… na mtoto wake ambao wanaishi katika mtaa wangu na wameahidi kutimiza wajibu wao mbele yangu.

Jina …………………………………………………………….. Sahihi: ……………………

Muhuri: ……………………………………………………… Tarehe: ……………………

Scanned with CamScanner

**FOMU "C"**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REGIONAL/DISTRICT MEDICAL OFFICER – MJIMWEMA HOSPITAL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**From**

**Part A:**

To the Medical Officer,

……………………………………………………………

……………………………………………………………

……………………………………………………………

Mr./Mrs./Miss ……………………………………………………………… (Name in full)

Please examine the above named as to his /her physical and mental fitness for a full time Teacher Training/Secondary education. The examination should include the following categories (I – IV) or sub – category of which will render the applicant ineligible in case of defect.

1. a) eye – sight
   b) Hearing
   c) Limbs
   d) Venereal diseases
   e) Leprosy
   f) Epilepsy
2. Neuroses
3. Pregnancy (Girls)
4. Other serious cases/diseases

**Part B: Medical certificate**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training/secondary education

1.
   a) Eye – sight ……………………………………………………
   b) Hearing ……………………………………………………
   c) Limbs ……………………………………………………
   d) Speech ……………………………………………………
   e) Venereal diseases ……………………………………………
   f) Leprosy ……………………………………………………
   g) Epilepsy ……………………………………………………
2. Neuroses ……………………………………………………………
3. Pregnancy (girls) ……………………………………………………
4. Other serious cases/diseases ……………………………………………

Date: …………………………  Signature: ……………………………

Station: …………………………  Designation: ……………………………

Scanned with CamScanner